# JESHI LA KUJENGA TAIFA

Simu ya Upepo: "JKT"
Simu ya Mdomo: +225-22-27582/8
Telefax: +255-22-2780048
Tovuti: www.jkt.mil.tz
E-mail: info@jkt.mil.tz

Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa
Sanduku la Posta 2963,
**Dodoma,** Tanzania
06 Nov, 2025.

## TAARIFA KWA UMMA

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), linaendelea kutekeleza majukumu yake ya Malezi ya Vijana, Uzalishaji Mali na Ulinzi tangu kuasisiwa kwake tarehe 10 Julai, 1963.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, JKT limekuwa na utaratibu wa kutoa taarifa zinazohusu shughuli zinazofanywa na JKT pamoja na Vijana wanaopatiwa Mafunzo ya JKT kupitia Vyombo mbalimbali vya Habari, Mitandao ya kijamii hapa nchini, Tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.mil.tz pamoja na mitandao ya kijamii ya JKT ambayo ni Instagram **jkttanzania**, Facebook **JKTTanzania**, Twitter (X) ni **JKTonlinetz** na Youtube **@JKTTanzania**.

Hivi karibuni kumejitokeza baadhi ya watu kufungua akaunti za kughushi (fake) katika mitandao mbalimbali ya kijamii kwa kutumia Jina, Nembo na rangi za JKT na kuaminisha umma kuwa akaunti hizo ni za JKT.

Akaunti hizo zimekuwa zikipakia maudhui mbalimbali yenye kuleta taharuki kwa jamii kuhusiana na shughuli zinazofanywa na JKT.

JKT linawataka wahusika wote waliofungua mitandao ya kughushi kwa kutumia jina la JKT, Nembo ya JKT, rangi za JKT, namba za vikosi, majina ya vikosi na makambi ya JKT kuzifunga mara moja akaunti hizo, Yeyote atakayepatikana akiendelea kutumia akaunti hizo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), linawakumbusha wananchi kuendelea kupata taarifa sahihi zenye uhakika zinazolihusu JKT kutoka Makao Makuu ya JKT kupitia Vyombo vya Habari, Mitandao ya Kijamii, Tovuti ya JKT na mitandao ya kijamii ya JKT iliyotajwa hapo juu.

**Imetolewa na:**
**Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,**
**Makao Makuu ya JKT**

MAKAO MAKUU YA JESHI LA KUJENGA TAIFA